Ulul Amr Ni Nani

Ulul Amr Ni Nani

Sayyid Sa'eed Akhtar Rizvi

Kimetafsiriwa na
Dhikiri U M Kiondo

Al-Islam.org

Author(s):

Sayyid Sa'eed Akhtar Rizvi [1]

Makala hii inatupa ufahamu kuwa viongozi wa dini ya kiislamu baada ya Mtume Mtukufu [s] ni kina nani. Pia inafafanua kwa aya za Qur'ani na Hadithi zinazoeleza utii kwa viongozi hawa.

Get PDF [2] Get EPUB [3] Get MOBI [4]

Translator(s):

Dhikiri U M Kiondo [5]

Utangulizi

Waislamu wamegawanyika makundi wawili kuhusu maana ya maneno "Ulul-Amr" yaliyotumika katika Aya ya 59 ya Surat An-Nisa.

Wako wasemao kuwa maana ya maneno haya ni "Watawala kutoka miongoni mwenu" - yaani watawala wa Kiislamu; na hii ndio tafsiri ifuatwayo na Waislamu walio wengi (Masunni).

Wako wengine wasemao kuwa, maana ya maneno hayo ni "Makhalifa (au Maimamu) Ma'asumiin (Watakatifu) Walioteuliwa na Allah kushika mahali pa Mtukufu Mtume [s] baada ya yeye Mtume [s] kuondoka. Hii ndio tafsiri ifuatwayo na Mashia-Ithna-ashariyah.

Kutoafikiana huku ni tatizo lihitajilo kutatuliwa kwa njia fulani. Kwa vile msingi mkuu wa Uislamu ni kutumia akili, inatulazimu kuutumia, msingi huu huu katika suala hili.

Maneno yafuatayo ni maelezo ya Ndugu yetu Sayyid Saeed Akhtar Rizvi aliye Mhubiri Mkuu wa Misheni yetu, akijaribu kulitatua tatizo hili kwa njia hii ya kutumia akili na kwa kuzichunguza aya nyingine za Qur'ani. Tunategemea kuwa, Insha-Allah wewe msomaji wetu nawe utafaidika kutokana na kijitabu hiki.

Mwisho tunamwomba Allah Atujaalie Tawfiq katika kuyasoma maneno Yake na kupata maana yake halisi itakayotuongozea kwenye Mwongozo wake halisi - Amin.

"Ulul Amr" Ni Nani?

Allah Anasema katika Kitabu chake kitukufu:

"Enyi mlioamini Mtiini Allah, na mtiini Rasuli (***Wake Muhammad***) ***na Wale waliopewa mamlaka kutoka miongoni mwenu, ……*** (***Qur'ani, 4:59***)

Aya hii inawawajibisha Waislamu aina mbili za utii. Kwanza, kumtii Allah; Pili kumtii Rasuli. Hii ina maana kwamba ni lazima "Ulul Amr" wawe na cheo kama kile cha Rasuli; au sivyo Allah asingetuamrisha kuwatii wao na kule kumtii Rasuli, katika Aya hii.

Kabla hatujaamua ni nani hao "Ulul Amr", ingetusaidia sana kama tungeitazama ile amri ya kumtii Rasuli [s], ili tuone jinsi amri hii inavyozunguka na kuenea kote-kote, na jinsi mamlaka ya Rasuli wa Allah [swt] ilivyo kuu.

Allah Anasema katika Qur'ani Tukufu:
"Na Hatukumtuma Rasuli yeyote ila atiiwe kwa idhini ya Allah…" (***Qur'ani 4:64***)

Ilibidi Manabii na Marasuli watiiwe na kufuatwa, sio kwamba hao wafuasi walitegemewa kukicheki kila kitendo cha Nabii na kuamua kipi kitiiwe na kipi kisitiiwe. Hii inathibitisha wazi wazi kwamba, Manabii na Marasuli walikuwa Ma'asumiin (Wasiotenda madhambi wala kukosea); na lau isingekuwa hivyo, Allah Asingewamrisha watu kuwatii Marasuli bila ya masharti yoyote.

Ziko Aya nyingi za Qur'ani Tukufu ambazo ndani yao Allah Anatuamrisha kumtii Rasuli, Akisema:

"Enyi mlioamini: Mtiini Allah na mtiini Rasuli....."

Tena Allah Anasema:

"Na mwenye kumtii Allah na Rasuli……" (***Qur'ani 4:69***)

Katika Sura hiyo hiyo inathibitishwa kwamba:

"Mwenye kumtii Rasuli amemtii Allah....."

Katika aya zote hizi za Qur'ani Tukufu na nyinginezo nyingi, utii kwa Allah umefanywa kuwa sawa na utii kwa Rasuli. Uthibitisho huu usingewezekana kama Manabii wasingekuwa Ma'asumiin na Watakatifu.

Sasa hebu ongezea aya hii ifuatayo katika aya tulizozitaja hapo juu:

"…Wala usimtii miongoni mwao mwenye dhambi." (***Qur'ani 76:24***)

Sasa picha imekamilika. Inabidi kuwatii Manabii. Watendao madhambi wasitiiwe: Hivyo, uamuzi ni

kwamba, Manabii si watenda madhambi. Kwa usemi myingine ni kwamba, Manabii ni Ma'asumiin (Watakatifu) na Wasiotenda Madhambi.

Hebu fikiria ni hali gani ambayo ingetokea kama Nabii yeyote yule angewasihi wafuasi wake wafanye kosa fulani au dhambi. Kwa vyo vyote vile hawa wafuasi waovu wangelaaniwa na kuipata ghadhabu ye Allah. Kama wakimtii Nabii yule na kuitenda ile dhambi wangekuwa wameihalifu amri ya Allah na hivyo wangefedheheshwa. Na kama kwa upande mwingine, wakimwasi yule Nabii, vivyo wangekuwa wameiasi amri ya Allah tuliyoitaja hapo juu yenye kuhusu kumtii Nabii. Hivyo yaonekana kwamba Nabii asiye Ma'asuum asingeweza kuwaletea watu wake cho chote kile ila fedheha na laana tu.

Tukimtazama hasa Mtukufu Mtume wetu [s] tunaona kwamba Allah Ametuamrisha Akisema:

"…Na anachokupeni Rasuli basi kipokeeni; na anachokukatazeni jiepusheni nacho…." (***Qur'ani, 59:7***)

Hii ina maana kwamba, kuruhusiwa au kukatazwa na Mtukufu Mtume [s] kila mara kulikuwa kukitegemeana na Mapenzi ya Allah na kila mara Alikupenda. Hii inathibitisha kwamba Mtukufu Mtume [s] alikuwa Ma'asum. Hakuna mtu awezaye kuwa na uhakika kabisa kabisa juu ya amri azitoazo mtu asiye Ma'asum.

Iko aya nyingine isemeyo:

"Sema (***ewe Rasuli wetu Muhammad***)***; Kama ninyi mwampenda Allah, basi nifuateni*** (***na***) ***Allah Atakupendeni na Atakughofirieni madhambi yenu…."*** (***Quran, 3:31***)

Katika aya hii, kumpenda Allah kumetegemezwa na kumfuata Mtukufu Mtume [s]. Pande zote mbili za mapenzi zimejumlishwa ndani yake. Kama unampenda Allah basi mfuate Mtume [s] kama ukimfuata Mtume [s] Allah atakupenda. Je, hii haionyeshi kwamba Mtukufu Mtume [s] alikuwa katoharika kabisa na kila aina ya dosari?

Si matendo yake tu, bali hata maneno yake yalikuwa ni amri ya Allah. Allah Anasema katika Qur'ani Tukufu:

"Wala hasemi (***huyu Rasuli Wetu Muhummed***) ***kwa matamanio yake. Sio hayo ila ni ufunuo uliofunuliwe kwake."*** (***Qur'ani, 53:3-4***)

Katika aya hizi tunaiona daraja ya hali ya juu sana ya Utakatifu awezayo kuifikiria mtu.

Vile vile ziko aya kadhaa katika Qur'ani Tukufu ambazo ndani yake maneno yafuatayo yametumiwa kwa ajili ye Mtukufu Mtume wetu [s].

"…. Rasuli kutoka miongoni mwao, awasomee ishara zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima……" (***Qur'ani, 62:2***)

Vipi Nabii ataweza kuwatakasa watu kutokana na madhambi na dosari iwapo yeye mwenyewe si Mtakatifu. Vipi mtu ataweza kuwafundisha wenzie hekima ikiwa yeye mwenyewe hana hekima imwezeshayo kupambanua baina ye ukweli na uwongo – Au lililo baya zaidi, pale akosapo uwezo wa nia ye kujizuia kutenda uovu pale anapoufahamu – Kazi ya Mtukufu Mtume [s] ilikuwa kuwafundisha watu Kitabu cha Allah. Hii ina maana kwamba yeye Mtukufu Mtume [s] alizijua amri za Allah.

Ilikuwa kwamba awatakase na kuwafundisha hekima; hii ina maana kwamba yeye mwenyewe alikuwa ne hekima na tohara.

Uthibitisho wa ukamilifu wa tabia zake unapatikana katika Qur'ani Tukufu, katika aye isemayo:

***"Na hakika* (*Wewe Rasuli Wetu Muhammad*) *une tabia njema adhimu"* (*Qur'ani, 68:4*)**

Mtu atendaye maovu hawezi kuistahili sifa hii. Aya zote hizi zaonyesha mambo mawili:

Jambo la Kwanza: Mamlaka ye Mtukufu Mtume [s] juu ya Waumini haina kikomo na ni yenye kuenea kote kote. Amri yoyote aitoayo, katika hali yoyote ile, mahali popote pale, na wakati wowote ule, ni wajibu kuitii bila ya swali lolote lile.

Jambo la Pili: Ni kwamba, yeye alipewa mamlaka kubwa sana kwa sababu ni "Ma'asum" (Mtakatifu) na katoharika kutokana na makosa, na madhambi. Isingekuwa hivyo, Allah Asingetuamrisha kumtii bila ya masharti yoyote yale.

Sasa katika aya hii (Qur'ani, 4:59), hawa "Ulul Amr" wamepewa mamlaka iliyo sawa kabisa na hii juu ya Waislamu, kwa sababu wote, "Rasuli" na hawa "Ulul Amr" wametajwa kwa pamoja, chini ya neno moja, Ati–'uu" (Mtiini) jambo ambalo laonyesha kwamba kuwatii "Ulul Amr" kuna maana ile ile ya kumtii Rasuli.

Hii yaonyesha kwamba "Ulul Amr" nao ni lazima wawe "Ma'asum" (Watakatifu), na waliotakasika kabisa kutokana na kila aina ya makosa, ne madhambi, au sivyo amri ya kuwatii wao isingeungwa na amri ya kumtii Rasuli [s].

Imamu wetu wa kwanza Amirul Mu'miniin Ali bin Abi Talib [a] alisema:

"Yeyote yule amwasiye Allah asitiiwe; na hakika utii ni wa Allah na Rasuli Wake na wale waliopewa mamlaka. Hakika Allah ameamrisha kumtii Rasuli kwa sababu yu Ma'asum, aliyetoharika na ambaye katu hatawaamuru watu kumwasi Allah; na hakika Ameamrisha kuwatii wale waliopewe mamlaka kwa sababu wao (nao) si watenda madhambi; wametoharika na hawawezi kuwaamuru watu kumwasi Allah."

(Kifungu hiki kimenukuliwa kutoka kitabu 'Ilalu Sharaye", kama kilivyonakiliwa katika Tafsiir Safi).

Kabla hatujaendelee zaidi, inatulazimu tueleze kuwa Waislamu wengi (Masunni) huyatafsiri maneno haye "Ulul Amr" kuwa na maana ye 'Watawala kutoka miongoni mwenu, yaani watawala wa Kiislamu. Tafsiri hii haina msingi wowote wa kihoja. Hoja yake imesimama katika msingi wa upotoshaji wa historia

ya Kiislamu. Waislamu wengi wamekuwa vibaraka wa wafalme na watawala wakiutafsiri Uislamu na Qur'ani kwa kurudia ili kuwaridhisha watawala wa kila zama.

Ulikuwepo wakati ambao ufalme ulikuwa aina ya pekee ya utawala iliyotumika. Katika zama hizo wanachuoni wa Kiislamu walikuwa wakiwatukuza wafalme na milki zao kwa kusema kuwa "Mfalme ni kivuli cha Allah" (Kana kwamba Allah ana kivuli). Siku hizi demokrasi ndio mtindo wa serkali na wanachuoni wa Kisunni hawachoki kuthibitisha katika maandishi yao, vitabu vyao na matoleo yao kuwamsingi wa Utaratibu wa serikali ya Kiislamu ni demokrasi. Huendelea hata kuthubutu kusema kuwa demokrasi ilianzishwa na Uislamu, wakisahau kabisa Jamhuri za miji ya Uyunani (Ugiriki) za zamani sana hata kabla ya Uislamu.
Katika nusu ya pili ya karne hii, ujamaa na ukomunisti vinazidi kuenea katika nchi zinazoendelea na wala sitashangaa kusikia kuwa wanachuoni wa Kiislamu wanajaribu kila wawezacho ili kuthibitisha kuwa Uislamu unafundisha na kujenga Ujamaa. Baadhi ya watu katika nchi ye Pakistani na mahali penginepo wamezua usemi usemao "Ujamaa wa Kiislamu." Maana hasa ya huu "Ujamaa wa Kiislamu", mimi sijui. Lakini mtu asishangae kuona kuwa katika muda wa miaka ishirini ijayo watu hawa hawa wataanza kudai kuwa Uislamu unafundisha Ukomunisti.

Mambo yote haya hubadilika ili kuudhihaki utawala wa Kiislamu.

Miaka michache iliyopita katika mkutano wa Waislamu uliofanyika katika nchi ya Kiafrika, ambao rais wa nchi hiyo alikuwa mgeni wa heshima, kiongozi wa Kiislamu alisema katika hotuba yake kuwa Uislamu unafundisha "Mtiini Allah, Mtiini Rasuli na watawala wenu'.

Katika Jibu lake, rais huyo (ambaye aliheshimiwa ulimwenguni pote kuwa yu kiongozi mwenye hekima na ambaye alikuwa ni Mkristo wa Kanisa Katoliki), alisema kuwa alipendezewa sana na hekima iliyomo katika amri ye kumtii Allah na Rasuli wa Allah, lakini hakuweza kuelewa hoja za amri ya kuwatii watawala wenu. Je, vipi iwapo mtawala huyo atekuwa mdhalimu na mwonevu? Je, Uislamu unaamrisha kumtii mtawala huyo kabisa kabisa bile ye kumpinga?

Hakika swali hili la kihekima linahitaji jibu la kihekima vile vile, wala haliwezi kutupiliwa mbali. Ukweli ni kuwa kiongozi yule wa kidini aliyesema vile, kasema kutokana na kuitafasiri vibaye Qur'ani. Historia ya Kiislamu imejaa majina ya watawala ambao udhalimu wao, uasherati wao na uonevu vimeiiharibu jina la Uislamu. Watawala kama hao kila mara wamekuwepo na bado wapo na watakuwepo hata pengine zaidi ya hao.

Ili kukupa mifano michache:

Yazidi bin Muawiyyah: Alikuwa Khalifa wa Uislamu. Lakini imani yake na tabia zake vilikuwaje? Yeye alikataa kabisa kumwamini Mtukufu Mtume [s]. Alionyesha wazi wazi imani yake katika Shairi lake lisemalo:

"Bani Hashim (Mtume [s] na Ahlul-Bait wake) walivumbua mbinu za kupatia milki. Kwa hakika

hakukuwepo na habari zozote zitokazo kwa Mwenyezi Mungu wala Ufunuo wowote."

Yazid hakuamini siku ya Mwisho. Anasema:

"Enyi wapenzi wangu (msiamini kuwa mtakutana nami baada ya kufa kwangu maana) yale walivyokuambieni kuhusu kufufuliwa baada ya kufa, kwa ajili ya Hukumu ni uzushi uufanyao moyo uzisahau fahari (za ulimwengu huu wa kweli)."

Baada ya kuupata Ukhalifa, aliidhihaki Sala ya Kiislamu waziwazi; akaonyesha kutoiheshimu dini kwa kuwavisha mbwa na ngedere mavazi ya viongozi wa kidini. Kamari na kucheza na madubu vilikuwa michezo yake ya kawaida. Alitumia muda wake wote katika kunywa kila mahali bila ya kusita; hakuwa na heshima kwa mwanamke yeyote na hata 'mahramu' wake kame vile mama, umbu, shangazi, mama mdogo na binti. Hawa wote walikuwa sawa na wanawake wengine mbele yake.

Mauwaji ya watu wa Nyumba ya Mtume [s] aliyoyafanya yanajulikana sana. Ulimwengu unafahamu kabisa yale yaliyotokea huko Karbala na jinsi Imamu Husayn [a] na masahaba wake na ndugu zake (akiwemo mtoto mwenye umri wa miezi sita) na jinsi wote hawa walivyokufa kishahidi mnamo tarehe 10 ya Muharram (Mfunguo 4) mwaka 61 A.H. jinsi watukufu hao walivyowekwa na njaa na kiu tangu tarehe 7 hadi 10 ya mwezi huo; jinsi mahema yao yalivyochomwa na jinsi familia yake (wakiwemo wanawake, watoto na mwanawe aliyekuwa mgonjwa sana) walivyofanywa mateka na kupelekwa Kufa na baadaye kupelekwa Demeshki; jinsi walivyotiwa jela kwa mwaka mzima kabla ya kufunguliwa. Mambo haya yanajulikana sana na hayana ulazima wa kuelezwa kwa kirefu hapa.

Baada ye mauwaji ya Karbala, Yazid alituma jeshi lake kwenda Madina. Mji huo Mtakatifu wa Mtume [s] ulitekwa nyara. Wasichana bikira mia tatu; achilia mbali wanawake wengine, walinajisiwa. "Quarii" (Wasomaji wa Tajwiidi) wa Qur'ani mia tatu na masahaba mia saba wa Mtume [s] waliuwawa kikatili. Msikiti Mtakatifu wa Mtume [s] ulifungwa kwa muda wa siku kadhaa; jeshi la Yazid liliutumia msikiti huo kama banda la farasi wao. Mbwa waliingia msikitini humo na Mimbari ya Mtume [s] ilinajisiwa na wanyama hao. Mwisho amiri jeshi wa Yazid aliwalazimisha watu wa Madina kumkubali Yazid kwa kuapa kwa meneno haya:

"Sisi tu watumwa wa Yazid; ni juu yake kutupa uhuru au kutuuza katika soko la watumwa."

Wale waliotaka kuapa kiapo cha utii kwa Yazid chini ya masharti ya kuwa 'Yazid afuate Qur'ani na Hadithi za Mtume [s] waliuawa.

Baada ya hapo, kwa amri ya Yazid jeshi lilikwenda Makkah. Mji huo wa Allah ulio mtakatifu kuliko yote duniani, ulizingirwa. Jeshi hilo halikuweza kuingia mjini humo, hivyo ikabidi askari watumie teo (fumbewe au kombeo–silaha ya kivita ya zamani sana iliyotumika kwa kutupia mawe mazito katika sehemu zilizo mbali).

Kwa kutumia teo walitupa mawe na vijinga vya moto katika Kaaba. 'Kiswa' (yaani nguo iifunikayo Kaaba

ikaungua na sehemu ya jengo hilo takatifu ikaanguka.

Na sisi tunategemewa kuamini kuwa Yazid alikuwa mmoja wa 'Ulul Amr' ambae kumtii kulikuwa wajibu kama kule kwa Mtume [s].

Walid Na Harun Rashid

Na haikukomea hapo tu. Inaonyesha kuwa matendo haye yalikuwa yakitendeka mara kwa mara. Walid bin Yazid bin Abdul Malik alikuwa Khalifa mwingine wa ukoo wa Bani Umayyah. Yeye alikuwa mlevi. Usiku mmoja alikesha akinywa pombe na mmoja wa suria wake hadi waliposikia Adhana ya Sala ya Alfajiri. Walid akaapa kuwa yule suria wake atasalisha. Hivyo yule suria akavaa joho la Khalifa na akasalisha katika hali ile ya ulevi na uchafu.

Siku moja Walid alimwona binti wake msichana wa miaka kumi hivi ambae bado hajaolewa na akamkera sana kwa kumtaka mapenzi. Mwanamke mtumishi wake alikuwepo pale kakaa. Yule mwanamke akasema kuwa (hakuwa Uislamu ule alioufanya Khalifa bali) ilikuwa dini ya Majus. Walid akajibu:

"Mtu anayejali ndimi za watu, hufa katika hali ya masikitiko; na mtu athubutuye kupata fahari zote."

Harun Rashid, Khalifa mashuhuri atajwaye katika kitabu kiitwacho "Alfu lela-u-lela" anayedhaniwa na wanahistoria wa Kiislamu kuwa ni mmoja wa Makhalifa wakubwa, alitaka kulala na suria wa baba yake aliyefariki. Yule mwanamke alisema kuwa isingeliwezekana kwa sababu alikuwa mama yake wa kambo. Harun Rashid alimwita Qadhi Bwana Abu Yusuf na kumtaka atafute njia ya kumtoshelezea haja yake. Qadhi huyo akasema:

"Yeye (mwanamke) alikuwa mjakazi tu. Je, wewe utakubali vyo vyote vile asemavyo? Hapana. Usikubali kila asemacho kuwa ni kweli."

Hivyo Khalifa huyo alitosheleza matakwa yake na mwanamke huyo. Bwana Ibn Mubaraka anasema:

"Sifahamu ni nani miongoni mwa watu hawa watatu aliyekuwa akishangaza sana, Khalifa anayechovya mkono wake katika damu na mali za Waislamu na ambaye hakumstahi mama yake wa kambo; au mjakazi aliyekataa kutosheleza haja ya Khalifa; au Qadhi aliyemruhusu Khalifa kumfedhehesha baba yake na kulala na yule Suria aliyekuwa mama yake wa kambo."

Nasi twaambiwa kuwa watu hao walikuwa 'Ulul Amr' waliotajwa katika aya hii.

Hebu ngoja tuirudie ile sentensi iliyoandikwa mwanzoni mwa habari hii. Kama Allah angetulazimisha kuwatii wafalme kama hawa, hali mbaya ingetokea kwa Waislamu. Waislamu wangeghadhibikiwa na

Allah, kwa chochote kile wakifanyacho. Iwapo watawatii watawala hawa, watakuwa wameasi Amri ya Allah isemayo;

"Wala msimtii miongoni mwao mwenye dhambi……." (***Qur'ani 76:24***).

Na iwapo watawaasi watawala hao, watakuwa vile vile wameiasi amri ya Allah ya kuwatii watawala wa Kiislamu."

Sasa, kama tukiikubali tafasiri ya Masunni, itaonekana kuwa Waislamu watapata laana ya milele iwapo watawatii au watawaasi watawala wao wasio 'Ma'asum.'

Vile vile wako watawala we Kiislamu wa imani na madhehebu mbali mbali. Wako Shaafi, Mawahhabi, Maliki, Hanafii na vile vile wako Shia na Ibadhi. Kwa kutegemeana na tafsiri hii, Masunni waishio katika nchi ya Sultani we Kiibadhi (kama vile Masqat) itawabidi wafuate mafundisho ya Kiibadhi; na wale waishio katika nchi ya Kishia (kama vile Iran) itawabidi wafuate mafundisho ya Kishia.

Je, watu hawa wanao uthibitisho wa nia zao wa kuifuata tafsiri yao kwa kadri ya hoja zake?

'Mufassir' mashuhuri wa Kisunni Imamu Fakhruddin Razi, ilimbidi akubali katika kitabu chake kiitwacho 'Tafsiir Kabir', kuwa aya hii inathibitisha kuwa 'Ulul Amr' ni lazima wawe 'Ma'asum'. Hoja alizozitoa ni kuwa Allah Amewaamrisha wanaadamu kuwatii "Ulul Amr" bila ya kutoa masharti yoyote; hivyo basi ni lazima "Ulul Amr" wawe 'Ma'asum'. Kwa sababu, iwapo upo uwezekano wa wao kufanya dhambi yoyote ile (na hali kufanya dhambi kunakatazwa) ingekuwa na maana kuwa mtu angelazimika kuwatii na vile vile kuwaasi katika tendo hilo (lililo dhambi),na hali jambo hili haliwezekani. Hivyo Bwana Fakhruddin Razi akabunia njia nyingine yakusema kuwa taifa la Kiislamu kwa ujumla ni 'Ma'asum'.

Tafsiri hii ni yake yeye tu, maana hakuna mwanachuoni mwingine wa Kiislamu aliyeitumia njia hii, na wala haimo mwenye msingi wa Hadithi yoyote ya Mtume [s].

Hakika inashangaza kuona kuwa, Imamu Fakhruddin Razi anakubali kuwa kila mtu wa taifa lile (yaani taifa la Kiislamu) si Ma'asum; na vivyo bado anadai kuwa jumla yao ni Ma'asum.

Hata mtoto wa shule ya msingi anafahamu kuwa 200a + 200a itakuwa 400a na wala si Ix.

Lakini tunatakiwa tuamini kuwa watu milioni 70 wasio Ma'asum ukiongeza wengine milioni 70 wasio Ma'asum utapata Ma'asum mmoja. Mshairi mmoja wa pande za Asia, Bwana Iqbal alisema:

"Akili za punda 200 haziwezi kutoa wazo la mtu mmoja."

Ni wazi kuwa uamuzi wa Imamu Razi kuwa 'Ulul Amr' ni lazima wawe Ma'asum, unatokana na elimu aliyokuwa nayo, lakini usemi wake kuwa "Ma'asum" maana yake ni taifa la Kiislamu, unatokana na chuki fulani.

Vile vile hakuacha kuonyesha wazi kuwa Aya yenye neno 'Minkum' (toka miongoni mwenu) inaonyesha

kuwa hao 'Ulul Amr' watakuwa ni sehemu ya taifa la Kiislamu, na wala sio taifa zima la Kiislamu.

Na kama taifa zima la Kiislamu lingetiiwa, basi ni nani ambaye angelibakia kutii?

Sasa turudi kwenye tafsiri sahihi ya Aya hiyo hapo juu.

Imamu Ja'far Sadiq [a] alisema kuwa aya hii iliteremshwa kuhusu Hadhrat Ali bin Abi Talib [a], Imamu Hasan [a] na Imamu Husayn [a].

Mtu mmoja alipomsikia Imamu Ja'far As-Sadiq [a] akisema hivyo, alisema kuwa watu husema kuwa mbona Allah Hakuyataja majina ya Ali na jamii yake katika kitabu chake?

Imamu Ja'far Sadiq [a] akasema: "Waambie kuwa, ililetwa amri ya Sala, lakini Allah hakutaja rakaa 3, au 4 na ilikuwa ni kazi ya Mtume wa Allah [s] kueleza kwa kirefu. Na tena Zakaat iliamrishwa lakini Allah hakueleza kuwa ilikuwa itolewe dirham moja katika kila dirham arobaini; na ni Mtume wa Allah [s] aliyeeleza. Hija iliamrishwa vile vile, lakini Allah Hakuamrisha kufanya Tawafu mara 7. Mtume wa Allah [s] ndiye aliye eleza kuwa tufanye Tawaf tufanyapo Hija. Aya hii izungumziayo juu ya 'Ulul Amr' mfano wake ni kama aya zihusuzo mambo tuliyoyataja hapo juu.

"Mtiini Allah na mtiini Rasuli na wale walio na mamlaka toka miongoni mwenu" na (hii aya) iliteremshwa kuhusu Hadhrat Ali [a] na Hasan [a] na Husayn [a]. (Uthibitisho huu umeandikwa katika kitabu kiitwacho 'Tafsiir Safi kama ulivyonakiliwa kutoka katika kitabu kiitwacho Kafi na kitabu kiitwacho Tafsiir Ayyashi.)

Katika kitabu kiitwacho "Kifayat-ul-Athar" iko hadithi iliyopokewa kutoka kwa Jabir bin Abdallah Ansari, ielezayo aya hii. Hadithi hiyo inasema kuwa, ilipoteremshwa aya hii Bwana Jabir alimwuliza Mtume [s] akisema:

"Tunamjua Allah na Mtume [s] lakini ni nani watu hawa walio na madaraka ambao utii kwao umeungwa pamoja na utii kwa Allah na wewe - Mtume [s] akamjibu: "Hao ni makhalifa wangu na Maimamu wa Waislamu baada yangu. Wa Kwanza ni Ali, kisha Hasan, Kisha Husayn, kisha Ali bin Husayn, kisha Muhammad bin Ali ambaye katika Taurat ameitwa Baqir. Ewe Jabir! Wewe utamwona. Umwonapo nitolee salaamu zangu kwake. Atarithiwa na mwanewe Ja'far Sadiq - Mkweli, kisha atafuatia Musa bin Ja'far, kisha Ali bin Musa, kisha Muhammad bin Ali, kisha Ali bin Muhammad, kisha Hasan bin Ali, kisha Muhammad bin Hassan.

"Yeye (Muhammad bin Hasan) atauteka ulimwengu wote toka Mashariki hadi Magharibi. Wakati wote atakaokuwa katika Ghaibu (kutoonekana katika macho ya wafuasi na marafiki zake, imani ya Uimamu wake itabakia katika nyoyo zile tu ambazo Allah kazijaribu kuhusu imani zao."

Hadithi hii imenakiliwa kutoka vitabu vya Kishia. Waandishi wa Kisunni wameiandika Hadithi hii kwa kifupi, lakini ziko Hadithi nyingi za Kisunni zizungumziazo kuhusu hawa Maimamu kumi na wawili. Msomaji anaombwa asome Sura ya 77 ya kitabu kiitwacho 'Yanabi-ul-Mawaddah' cha Sheikh Hafidh Sulaiman bin Ibrahim Qanduzi Hanafi, aliyefariki mnamo mwaka 1294 Hijiriya.

Kwanza kabisa Sheikh huyo ameinakili ile Hadithi mashuhuri sana isemayo:

"Watakuwepo Makhalifa kumi na wawili, wote kutoka miongoni mwa Makuraishi."

Hadithi hii imeandikwa katika vitabu vingi sana miongoni mwa vitabu hivyo vikiwemo vitabu vya Mabwana Bukhari, Muslim, Abu Dawuud na Tirmidhi.

Kisha amenakili Hadith nyingi sana zithibitishazo kuwa, Mtume [s] alisema:

"Mimi, Ali, Hasan, Husayn na watu tisa kutokana na kizazi cha Husayn ni Safi na Ma'asum."

Vile vile amenakili Hadithi isemayo kuwa Mtume [s] alimwambia Imamu Husayn [s]:

"Wewe ni Sayyid mwana wa Sayyid, ndugu wa Sayyid; Wewe ni Imamu, mwana wa Imamu, ndugu wa Imamu, wewe ni uthibitisho (wa Allah), ndugu wa uthibitisho wa Allah na baba wa thibitisho tisa (za Allah), ambao wa tisa wao atakuwa Mahdi."

Baada ya kunakili hadithi nyingi za aina hiyo, anaendelea kusema:

"Wanachuoni wengi wamesema kuwa Hadithi (zionyeshazo kuwa Makhalifa baada ya Mtume [s] watakuwa kumi na wawili) ni mashuhuri, zitokanazo na Asnaad (mnyororo [mlolongo] ya watu waliosikia Hadithi hiyo mmoja toka kwa mwingine) nyingi. Sasa kutegemeana na muda upitavyo na matokeo ya kihistoria, tunajua kuwa, kwa Hadithi hii, Mtume [s] alikuwa na maana ya Maimamu kumi na wawili kutokana na Ahlul-Bait na Dhuria wake."

Kisha ametoa sababu zithibitishazo kuwa Hadithi hizi haziwezi kuwa zinazungumzia kuhusu Khalifa Rashidiin wanne, wala wafalme kutoka katika nyumba ya Umayyah wala wale watokao katika nyumba ya Abbas.

Mwisho kabisa anasema:

"Hivyo basi, njia ifaayo tu, kwa kuitafsiri Hadithi hii ni kukubali kuwa inazungumzia kuhusu Maimamu kumi na Wawili kutokana na Ahlul-Baiti wa Mtume [s] na Dhuria wake, kwa sababu walikuwa watu waliokuwa na Elimu zaidi katika zama zao, waliomwongopa Allah zaidi, wachamungu zaidi, waliokuwa wa kiwango cha juu sana katika nasaba yao, wabora zaidi katika matendo, watukufu zaidi mbele ya Allah, na Elimu yao ilitokana na jadi zao (Mtukufu Mtume [s]), kupitia kwa baba zao, na kwa njia ya kurithi na mafunzo ya moja kwa moja kutoka kwa Allah."

Sasa tunajua ni nani wale 'walio na mamlaka", na sasa tunaweza kuona wazi wazi kuwa suala la kuwatii watawala waonevu na dhalimu halihusiani hata kidogo na aya hii. Waislamu hawawajibishwi kwa aya hii kuwatii, "Watawala wenu" ambao wanaweza wakawa wadhalimu, waonevu, wajinga, wachoyo na waliojitumbukiza katika uasherati. Waislamu wanaamrishwa na aya hii kuwatii Maimamu 12 ambao wote walikuwa watakatifu na wote walitakasika na kila aina ya mawazo au matendo mabaya. Kuwatii

Maimamu hawa hakuna hatari yoyote. Kunatuliano kutokana na hatari ya aina yoyote; kwa maana Maimamu hawa hawatatoa amri yoyote kinyume cha Penzi la Allah na watawafanyia binaadamu wote upendo, haki na usawa.

Source URL: https://www.al-islam.org/ulul-amr-ni-nani-sayyid-saeed-akhtar-rizvi#comment-0

Links

[1] https://www.al-islam.org/person/allamah-sayyid-saeed-akhtar-rizvi
[2] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/49785
[3] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/49785
[4] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/49785
[5] https://www.al-islam.org/person/dhikiri-u-m-kiondo